TUAMBIE UNAFIKIRI NINI KUHUSU MWONGOZO HUU!

# Kanuni za Ufundishaji

MWONGOZO 1

## Usimamizi wa Serikali na Matumizi ya Programu

### UTANGULIZI

**Hakuna programu kubwa ya misingi ya kusoma na kuhesabu (FLN) inaweza kuwa na ufanisi bila usimamizi wa serikali. Kwa msingi huo, ni bahati mbaya mara nyingi wafadhili, washauri wa kitaalamu, na watekelezaji wanakuwa hawana ufanisi katika kutengeneza mazingira yanayohitajika kwa serikali kuweza kusimamia. Kushindwa huku mara nyingi huondoa uwezekano wa uendelevu mzuri wa kuingilia kutoka mwanzo. Matokeo ya kujifunza ni magumu kubadilika, kwa kuwa hii inahitaji makumi kwa maelfu ya walimu kubadilisha mbinu zao za ufundishaji, lakini serikali ikisimamia na walimu wengi wakitumia programu hii, matokeo katika kujifunza yanawezekana. Mwongozo huu unawasilisha michakato ya hatua kwa hatua ili kuhakikisha kwamba serikali iliyovutiwa inaweza kutoa usimamizi na kuongeza utumiaji wa programu.**

**Katika baadhi ya kesi, serikali inaweza kutoa fedha na kuongoza programu ya FLN, kuweka programu hii kwa mafanikio kwa kutumia miundo na mifumo iliyopo. Kwa mfano, mifumo ya elimu ya Sobral, Brazil, na Puebla, Mexico, ilipata mafanikio makubwa katika ujifunzaji wakati programu ikiongozwa moja kwa moja kwa kutumia mifumo ya serikali. Uingiliaji huu uliunganisha malengo ya programu ya FLN na malengo ya jumla ya jamii. Mara nyingine, wafadhili wa nje wanaweza kutoa msukumo wa awali na msaada wa kifedha. Katika tukio lolote, ushiriki mzuri na matumizi ya mafunzo vitachangia kwa kiasi kikubwa katika mafanikio ya programu; Jambo hii litachukua muda lakini ni muhimu.**

Fanya mchakato wa mapitio ya Taasisi kabla ya kuendelea na hatua zozote katika muhtasari huu. Mapitio ya wizara ya elimu yatakueleza kuhusu:

1. **mfumo wake rasmi wa utawala** na jinsi wafanyakazi wake wanavyofanya maamuzi;
2. **mfumo wake wa utawala usio rasmi**— ambao watu hupata madaraka, uhusiano wao na wafanya maamuzi, na mifumo mingine ya kijamii wanayohusiana nayo na
3. **uhusiano mwingine wowote taasisi nyingine**.

   Kitu cha kufurahisha zaidi ni mwelekeo mkuu wa kisera wa wizara na uhusiano wake na wizara ya fedha, utumishi wa umma, mashirika ya umma (ikijumuisha taasisi zinazohusika na mitaala, kitengo cha usimamizi wa walimu na mifumo ya tathmini), vyama vya walimu, vyama vya kitaaluma vya walimu, na taasisi nyingine za kiraia.

Hata kama hakuna mtu aliyefanya zoezi la kufanya mapitio mwanzoni mwa programu ya kusoma au kuhesabu au wakati ikibuniwa, mapitio hayo bado yanaweza kuthibitisha kuwa ya msaada katikati ya utekelezaji.

USIMAMIZI WA SERIKALI HATUA YA 1

### ANZA KWA KUSIKILIZA

Je, viongozi wa elimu ya ufundi wana vipaumbele gani katika nchi? Programu za FLN zilizofanikiwa zitatoa vipaumbele na mahitaji hayo. Ni rahisi kupata barua rasmi ya ruhusa. Kinachotofautisha programu ya FLN iliyofanikiwa na ile ambayo haijafanikiwa ni pale programu inapoonekana inakidhi mahitaji ya viongozi wakuu Iwe hiyo inaongozwa na timu maalum ndani ya serikali au inatokana na ushirikiano wa pamoja na kitaalamu ya kitaalamu nje ya serikali, kazi kubwa ni kuelewa ni nani wafanya maamuzi wakuu na vipaumbele vipi ni muhimu zaidi kwao.

Kama ilivyoonyeshwa hapo juu, kufanya mapitio ya kitaasisi ya wizara na taasisi nyingine za serikali, ikiwa ni pamoja na wizara ya fedha, vyama vya walimu, na taasisi inayowakilisha wasimamizi wa walimu – yatafichua watu wenye ushawishi. Kama muhimu ulivyoonyeshwa hapo juu, katika muktadha fulani, mapitio ya kitaasisi yatafichua ni nani wanaokwaza.

**Wapangaji lazima wasikilize kwa makini ili waelewe viongozi wa serikali wanataka nini, nani anafanya maamuzi ndani ya muundo wa serikali, na wapi zipo nguzo za nguvu ndani ya vitengo mbalimbali vya wizara ya elimu**. Kwa mtazamo tofauti kidogo, mafanikio ya programu ya FLN yanategemea kuelewa iwapo na jinsi malengo ya ajira ya viongozi hawa wakuu yanafungamana na malengo ya programu.

Pointi ya kuzingatia hapa, wakati ambapo programu inaongozwa kwa kusikiliza, itakuwa rahisi zaidi kuepuka migogoro juu ya maana au istilahi zenye utata. Kwa mfano, programu lying zinazopewa fedha na mfadhili mkubwa zimejikita katika *kusoma*, ambapo taasisi za mitaala zilizokuwa zikizisaidi zilipendelea kusoma*kusoma* ikujumuisha pia kuandika. **Kutohoa istilahi kwa urahisi kulingana na matumizi yanayopendelewa ya nchi kunaweza kuepusha kiasi fulani cha utata au uchungu**.

USIMAMIZI WA SERIKALI HATUA YA 2

## KUZA MAHITAJI KWA KUJIBU VIPAUMBELE VYA JAMII

Programu ya FLN yenye ufanisi si tu inapaswa kuendana na vipaumbele vya watendaji wakuu katika mfumo, lakini pia:

- **Fungamanisha na mambo yanayowatia motisha za walimu** . Je, wanatathminiwaje na mambo gani huathiri mwelekeo wa ajira yao?
- **Ingiza vipaumbele vya kanuni za ufundishaji katika kile ambacho serikali tayari inataka kitokee na wakati wa kutokea**. Progrmu nyingi za FLN zilizotoka nje hutekeleza bila kuzingatia mitindo ya mipango ya serikali.
- **Elewa mzunguko wa bajeti kuu na uulize maswali muhimu kwa wakati unaofaa**. Uelewa huu utafanya maombi ya kibajeti pamoja na mipango na upangaji wa wataalamu kuwezekana.
- **Tazama na utumie maeneo ya sera**. Mchakato wa mipango ya sekta ya elimu hutoa fursa mbalimbali za kuzitumia. Maandalizi ya mpango wa sekta ya elimu ambayo hutokea kila baada ya miaka mingi na tathmini ya Pamoja ya sekta hutokea kila mwaka ndio fursa nzuri yay a kuiangalia sera Fursa nyingine, kama vile ahadi zilizotolewa na mwanasiasa, matakwa ya raia kwa matokeo bora ya elimu, au mabadiliko katika jinsi maofisa wa serikali wanavyosimamiwa.

Hata hivyo, si mbinu zote zenye ufanisi wa kuchochea mahitaji ya ufundishaji ni za kitaalamu. Mara nyingi zinategemea stadi laini, subira na uthabiti dhidi ya urasimu mkubwa wa Serikali na kuwashawishi kwamba kuboresha FLN ni jambo la kunufaisha pande zote. Progamu za FLN zenye ufanisi zimeweza kufanya kazi pamoja na washirika wa kiserikali ili ziongeze muda wa kufundisha, kuanzisha jumuiya za walimu za mikutano ya mazoezi kama sehemu ya wiki, na hata bajeti ya ununuzi na kusambaza vitabu vya wanafunzi kwa kutumia fedha na mifumo ya serikali. Kufanya kazi na serikali kunawezekana iwapo programu inafungamana na vipaumbele na mifumo yao. Kwa ufupi, ni rahisi kuogelea pamoja na mawimbi.

USIMAMIZI WA SERIKALI HATUA YA 3

## AJIRI WAFANYAKAZI WENYE MAARIFA NA WANAOHESHIMIKA

KUAJIRI NA KUCHAGUA WAFANYAKAZI WANAOFAA KWA AJILI YA KAZI HIYO NI MUHIMU

Kwa sababu ya mabadiliko mubwa ambayo mfumo utahitaji kufanyiwa ili kutekeleza programu iliyopachikwa na kiwango kikubwa, kuajiri na kuchagua wafanyakazi wanaofaa kwa ajili ya kazi hiyo ni muhimu. Ukweli huu hutumika iwapo programu inasimamiwa na mtekelezaji wa nje au kama serikali ina kitengo chake cha utekelezaji wa mradi.

Wafanyakazi hawa watahitaji kufanikisha jukumu la washauri wanaoheshimika kwa wafanya maamuzi ya kitaalamu. Kwa kesi za programu za nje, zinapaswa kuchaguliwa bila kupora wafanyakazi wa wizara ya elimu na taasisi zinazohusika; maofisa wastaafu wanaoheshimika wa wizara wanaweza kuhudumu katika jukumu hili pia. Kimsingi, maamuzi ya kuajiri yanapaswa kuanzia kwenye ramani ya kisiasa iliyojadiliwa hapo juu: Nani katika serikali anafanya maamuzi, na jinsi gani wajumbe wa timu wanaweza kuunganisha? Wanafunzi wenzako wa zamani na wafanyakazi wenzao wa maafisa wa wizara, ikiwa wana utaalamu, vipaji na ujuzi unaohitajika, mara nyingi hufanya kuwa washauri bora. Wafanyakazi waliofanikiwa bila shaka wanapaswa kujumuisha wataalam wa kitaalamu katika kusoma na kukuhesabu ambao hutoa michango ya muhimu jinsi mabadiliko haya ya uboreshaji wa elimu yanaweza kufanywa.

Wafanyakazi na washauri wanaoaminika wanaweza kuchukua jukumu la kuandaa "vikao vya awali" pamoja na wafanya maamuzi wakuu wa wizara. Katika vikao hivi, wanaweza kueleza jinsi shughuli ya FLN ilivyo na maslahi kwa afisa huyu mahususi wa serikali. Wafanyakazi hao pia wanaweza kutumia mtaji wao wa kijamii ili kutofautisha uingiliaji wa FLN unaopendekezwa kutoka programu za mwanzo ambazo mwenzake na serikali anaweza kuwa aliona zikija na kuondoka. Wanaweza kutetea wenzake ili kuamua kuwa programu hii ni ya kweli na ili kuwekeza mtaji wao katika mafanikio yake.

### USIMAMIZI WA SERIKALI HATUA YA 4

## KUZA MAWAZO YA MABINGWA

Programu za kanuni za ufundishaji zenye ufanisi zina mabingwa. Mabingwa si lazima wawe wafanyakazi wa Wizara ambao mwanzoni watakubali wazo hilo, lakini badala yake ni wale wenye ushawishi shauku ya mabadiliko.

Programu ya kanuni za ufundishaji ya FLN—ambayo wengi wataona kama ni kuhusu maandalio ya somo ya mwalimu na vitabu vya kiada vya wanafunzi—utakuwa na ufanisi ikiwa tu idadi kubwa ya shughuli zilizounganishwa zitatokea kwa ukubwa wa tofauti sana kuliko kawaida. Kwa kusema hivyo, itakuwa kiburi kudhani kuwa programu ya FLN kulingana na ushahidi bora wa kimataifa itafanya kazi kila mahali. Kazi ya kufanya ni kufahamishwa na ushahidi bora zaidi wa kimataifa, lakini kuhakikisha kuwa huu ni mpango mahususi wan chi unaojibu suluhu zinazopatikana nchini. Ni hakika, mawazo muhimu ya kukamilisha lengo hili na kuboresha matokeo tayari yanasambaa katika mfumo. **Jukumu la kiongozi wa FLN ni kupata nafasi ambapo mawazo hayo yote yanajadiliwa katika ngazi ya kitaifa, ili kukuza mawazo hayo ndani ya programu ya FLN, na kutoa shukrani kwa viongozi hao—mabingwa—ambao ndio wanaotoa mawazo hayo**.

Fikiria jinsi timu yako na programu vinaweza kusaidia kwa njia ambazo ni zaidi ya jukumu maalum la FLN lililopo ili kujenga uaminifu kwa wizara. Zingatia kutumia utaalamu wa timu yako ili kusaidia wizara kwa majukumu mengine katika sekta zingine ndogo ili kuonyesha thamani yenu.

### USIMAMIZI WA SERIKALI HATUA YA 5

## JENGA KWA USHAHIDI

Ushahidi hufanya tofauti. Fursa ya kuwasilisha programu hii ya kanuni za ufundishaji kwa Waziri kwa mara ya kwanza inaweza kuwa ni mpango mkubwa kwako (iwe unafanya kazi serikalini ama ni mdau wa nje), lakini unaweza kuwa wa tatu kati ya vikundi 10 tofauti vyenye mawazo mapya ambayo waziri atayasikia siku ya leo. Kuna matatizo mawili katika picha hii: (1) Hupaswi kwenda kuwasilisha programu, bali kusikiliza mawazo na matamanio; na (2) unaweza kuwezeshwa na ushahidi wa hali ya matokeo ya ujifunzaji ambayo hayajafikia matarajio, lakini pia kuhusu tatuzi ambazo zinapendekezwa kwa eneo la jamii ili kuondoa vikwazo vikuu kwa ujifunzaji bora. Je, ushahidi gani unaweza kutoa ili kutofautisha progrmau yako ya kanuni za ufundishaji na nyingine nyingi za nyuma ambazo zilikuwa na athari ndogo katika kujifunza?

Ushahidi wa sasa unaweza kuwa tofauti sana ndani ya serikali kuliko wafadhili au watafiti. Uzoefu unasema kwamba ushahidi kutoka kwenye majaribio ya elimu yanayodhibitiwa yasiyopangiliwa yanaweza kusaidia kwa ushawishi. Lakini maandiko yaliyochapishwa mara chache huwa na athari kubwa zaidi. Badala yake, mazungumzo bora zaidi ni grafu zinazoonyesha athari, pamoja na mahojiano ya walimu waliotekeleza, ushahidi wa kujionea madarasa yenye ufanisi, na safari za maeneo kuona jinsi programu inavyofanya kazi. Programu zenye ufanisi hazihitaji kuandika ziara zao za eneo, kwa sababu viongozi wa serikali wanaweza kueleza tofauti kati ya ufanisi na programu ambayo inafanya kazi kweli. Kuwa na viongozi waliotembelea shule na kusoma au kufanya kuhesabu za msingi pamoja na mwanafunzi katika shule ya kawaida kunaweza kuwa na athari kubwa katika kufanya maamuzi. Kiongozi mwandamizi wa Wizara ya Elimu ya Kenya, na mwenye shaka sana, mara kwa mara hakushawishiwa na takwimu na grafu za kuvutia zinazoonyesha matokeo ya majaribio ya PRIMR. Ilikuwa ni wakati wa ziara ya seti ya shule za vijijini, ambapo alipuuza taratibu za ziara hiyo na kutumia muda kusoma pamoja na mtoto mmoja mmoja, alishawishika juu ya uwezo wa PRIMR kuongezwa.

Ukaguzi unaoendelea na timu zinazotekeleza nchini kote ni njia ya kudumisha mazungumzo kuhusu jinsi ya kuboresha, kuruhusu timu kujifunza na kukabiliana na matokeo. Hata programu iliyobuniwa vyema inaweza kunufaika kwa kutafuta ufadhili wa pamoja, utafiti mdogo ili kujibu masuala ambayo viongozi wakuu wa serikali huibua. Uwekezaji huu mdogo unaweza kutoa faida kubwa kwa ubora wa programu na usimamizi wa serikali.

VIONGOZI WA SERIKALI WANAWEZA KUELEZA TOFAUTI KATI YA ZIARA YA MAONYESHO YENYE KITU KIDOGO NA PROGRAMU INAYOFANYA KAZI KWELI

USIMAMIZI WA SERIKALI HATUA YA 6

## TAFUTA VITUO VYA NISHATI

Kuelewa vituo vya nishati ni muhimu kwa kuoanisha matumaini ya mabadiliko na utashi wa kisiasa. Kila serikali ya kitaifa ina kituo zaidi ya kimoja cha kufanya maamuzi, hususan baina ya nchi ambazo zimegatua shughuli zake muhimu. Makundi ya Elimu ya Jamii ya Ndani hujumuisha wafadhili, asasi za kiraia na watekelezaji wa elimu na ni watendaji muhimu kuelewa jukumu na ushawishi wao katika kufanya maamuzi.

Mchakato wa kuchora ramani ya kitaasisi unaweza kuelezea kwa kina nani ana ushawishi juu ya sehemu za uingiliaji kati wa FLN, ambaye ndani ya taasisi hiyo ana nguvu ya kufanya maamuzi, na kuna unyeti gani kati ya kundi hilo na wengine katika sekta hiyo. Kwa maarifa haya, timu ya uingiliaji kati inaweza kuepuka vema kukamatwa na kutokukubaliana kusiko na utulivu kati ya huduma pinzani za serikali.

Miundo iliyogatuliwa kwa kawaida huwa na ngazi tofauti za ushawishi juu ya maboresho ya ufundishaji. Kulenga uwekezaji sahihi kwa kila ngazi, hivyo, ni muhimu.

Kwa mfano, kwa sababu ya uhusiano wa kifedha na ufahari, wafanyakazi wa mafunzo kutoka pande zote za Wizara mara nyingi huibuliwa kuwa kipaumbele cha juu, hata kama muundo wa programu utaona faida ndogo ya uwekezaji kama huo kulingana na matokeo yanayotarajiwa kutokana na maafisa wa mafunzo ambao wameunganishwa kwenye utekelezaji wa kanuni za ufundishaji. Kwahiyo, ili kuhakikisha gharama ya kumudu, programu ya FLN itahitaji kuvuka tofauti za maoni kwa makini kati ya vituo vya nishti. Chaguzi hizi zinaweza kuanzisha biashara, ingawa; kuna uwezekano kundi moja ndani ya serikali likawa adui wa uingiliaji kati iwapo wataona kuwa wanadharauliwa kwa kutoshirikishwa.

Nchi hutofautiana katika matabaka la watumishi wa umma wa ngazi ya kati waliopo kati ya waziri na mwalimu. **Bila kujali idadi ya matabaka, juhudi za utumiaji wa programu lazima zitatue si tu ngazi ya juu, lakini pia matabaka ya chini na uhalisia wa shughuli zao za kitaaluma za kila siku na motisha**.

UTUMIAJI WA PROGRAMU HATUA YA 1

## MAELEZO YA MAJUKUMU NA MOTISHA

Je, ni jinsi gani walimu, makocha, wasimamizi, na watumishi wa umma katika sekta ya elimu wanatathminiwa, na wamepewa majukumu gani ya kufanya? Kujua taarifa hii itaonyesha njia bora ya kuwahamasisha, na pia itaruhusu nadharia ya programu ya kanuni za ufundishaji kubalidilika ili ifungamane na motisha binafsi na za kikundi.

Cha kushangaza sana, maelezo ya majukumu, yanaweza kuwa moja ya vitu muhimu vya kutofautisha kati ya programu za kanuni za ufundishaji ambazo zinafanya kazi na zisizo fanya kazi. **Ni muhimu kwa programu zenye ufanisi za kanuni za ufundishaji kukagua maelezo ya majukumu, vigezo vya tathmini, na chati za kitaasisi, na kufanya kazi pamoja na washirika wa serikali ili kufungamanisha hati hizo zote**. Baadhi ya programu zenye ufanisi zaidi za kanuni za ufundishaji zimejikita kufanya kazi na serikali ili kubadilisha maelezo ya majukumu na vigezo vya tathmini. Juhudi hii inaweza kuwa rahisi kamavile kuthibitisha kwamba mahitaji yaliyopo kwenyemaelezo ya majukumu yanafungamana na lengo la program una kwamba malengo haya yanaweza kujumuishwa katika mapitio ya mwaka. Au inaweza kuhitaji kuboresha maelezo ya majukumu ili kusisitiza msaada wa ufundishaji, na kujadili ni jinsi gani muda uliotengwa kwa majukumu mapya utaathiri fidia.

Kitu cha karibu ya maelezo ya kazi ni tathmini ya ufanisi wa mtu binafsi. Wasimamizi wa serikali wanapotathminiwa kwa msingi wa uingiliaji kati wa kanuni za ufundishaji zinapotekelezwa kwa ufanisi, ndipo data zilizozalishwa na programu ya kanuni za ufundishaji (tazama Mwongozo wa 7 katika mfululizo huu, kwenye data, mifumo, na uwazi) inakuwa fedha ya thamani, mabadiliko ya motisha, na matokeo muhimu kuwezekana. Ikiwa mabadiliko haya yatafanyika katika mfumo mzima, wasimamizi wanaweza kuanza kuja kwenye mpango wa kanuni za ufundishaji ulioandaliwa ili kupata ushahidi wa jinsi mambo yanavyokwenda na kuchukua jukumu lao ili kuhakikisha kuwa maofisa wao wanatekeleza kwa ufanisi.

Lengo kuu ni kuwafanya maofisa hawa wafanye kazi kama mawakala wakuu wa mabadiliko wanaoongoza mjadala wa jinsi fedha za ugatuzi zinavyotumika, ili rasilimali zilizopangwa ziendane na utekelezaji wa mafunzo ya kila siku - ikiwa ni pamoja na uchunguzi wa darasani, mrejesho kwa walimu, na mikutano ya jumuiya ya mazoezi, kulingana na muundo wa programu ya kanuni za ufundishaji iliyoundwa. Haitatokea kwa kila muktadha kwa namna moja, lakini inawezekana kuhama kutoka kwenye uchunguzi wa maelezo ya kazi kwenda uongozi wenye mantiki katika ngazi za kitaifa na chini ikisisitiza ufundishaji bora na kujifunza zaidi. Kwa mfano, baadhi ya programu, zimefanya kazi na serikali ili kubadilisha kiasi cha muda wa ufundishaji uliopangwa kwa ajili ya masomo ya kusoma na kuhesabu, ili kuunganisha ujifunzaji wa walimu na mikutano ya tafakari kuwa majukumu ya kila wiki, na kuhakikisha kwamba ufundishaji masomo ya kanuni za ufundishaji huwa na kigezo cha tathmini.

MAELEZO YA KAZI YANAWEZA KUWA BAINA YA VITU MUHIMU SNA VINAVYOTOF-AUTISHA KATI YA PROGRAMU ZA KANUNI ZA UFUNDISHAJI AMBAZO ZINAFANYA KAZI NA ZILE ZISIZOFANYA KAZI

### UTUMIAJI WA PROGRAMU HATUA YA 2

## ELEWA WALIMU

Walimu wao wenyewe wana mengi ya kuchangia kwenye mazungumzo ya programu. **Programu zitapitia wakati mgumu iwapo hazijafanya majadiliano na walimu – ikijumuisha walioko maeneo ya vijijini – ili kuelewa kazi zao zikoje, ni vikwazo gani vya sasa kufikia mbinu za kufundishia zilizoboreshwa**, au jinsi walivyojibu kwa programu kubwa za mwanzo. Zaidi ya hayo, programu nyingi zimefanya makosa ya kutozingia jinsi walimu na watumishi wa umma wanaendelea, uhusiano walioanao walimu na asasi za kiraia, miundo inayowazunguka walimu, nani ana ushawishi juu ya tabia yao ya ufundishaji. Walimu ambao programu hii inapaswa kuwafikia inatakiwa kujumuisha idadi kubwa ya walimu, kwa kuzingatia jinsia, uandamizi, kabila na mahali. Kwa kuongezea, ni muhimu kuelewa mchango wa vyama vya walimu katika kuchangia kwenye mwenendo wa taaluma ya ufundishaji na mbinu za mabadiliko ya mwalimu.

Ushahidi kutoka muktadha mwingine unaweza kuwa pointi muhimu ya kuanzia, lakini programu za FLN zilizofanikiwa pia zitahusisha maarifa ya kina ya eneo husika ya uchumi wa kisiasa wa elimu katika nchi hiyo. Inamaanisha kujifunza jinsi kazi za ualimu zinaweza kubadilishwa ili zifungamane na maboresho mengine yanayotamaniwa, kama vile muda mwingi wa kufundisha na matumizi bora ya nyenzo mpya.

### UTUMIAJI WA PROGRAMU HATUA YA 3

## KUFANYA MAAMUZI YA KANUNI ZA KUFUNDISHIA

Kimsingi, kazi ya kuboresha kusoma na kuhesabu za msingi hutegemea kuinua ubora wa ufundishaji na kuunga mkono ufanyaji maamuzi wa ufundishaji wa walimu binafsi – makumi ya maelfu yao, nchini kote. Ikiwa asilimia kubwa ya walimu hao wanafundisha programu kwa ustadi, wataleta athari ya programu.

Je, ni ujumbe gani viongozi wa kitaifa na ngazi ya chini wanakuza baina ya walimu wao kuhusu umuhimu wa uwiano wa programu hii dhidi ya vipaumbele vingine vinavyoshindana? Inasaidia kuwa na uongozi wa kitaifa na wizara, na kiongozi wa elimu akizungumza kwa sauti moja kuhusu umuhimu wa kutekeleza uingiliaji kati wa FLN. Hata hivyo, muhimu zaidi ni uzoefu wa walimu binafsi. Haijalishi ni ujumbe gani wa kutoka juu unashirikishwa, katika nchi nyingi walimu wana kiasi kikubwa cha uharaka na uwezo wa kufanya maamuzi katika maamuzi yao ya kanuni za ufundishaji. **Viongozi wa programu wanapaswa kupima kwa umakini kiwango cha ugumu wa programu ya FLN kwa mwalimu dhidi ya kile ambacho walimu wamezoea kufanya. Programu amabayo mwalimu wanaiona kuwa ni ngumu sana itakuwa na uwezekano mdogo au kutokuwa na uwezekano kabisa wa kutekelezwa mara kwa mara.**

INASAIDIA KUWA NA RAIS, WAZIRI NA KIONGOZI WA ELIMU WA ENEO LA NDANI WAKIZUNGUMZA LUGHA MOJA KUHUSU UMUHIMU WA KUTEKELEZA UINGILIAJI KATI WA FLN

Kwa kufafanua zaidi, tunatoa mfano wa "mwalimu wanaobadilika" ulioonyeshwa kwenye Kielelezo cha 1. Wapiga kura wanaobadilika ni wapiga kura ambao hawashirikiani na chama fulani na wanaweza kushawishiwa katika mwelekeo mmoja au mwingine. Katika njia hiyo, wako kama walimu ambao wanaweza kushawishiwa ili kutekeleza programu hiyo. Ikiwa kiasi cha sehemu ya walimu ( **KIJANI** kikundi) waliovutiwa sana na kiko tayari kujaribu uingiliaji kati mpya hata kama ni ngumu. Sehemu nyingine ya walimu (the **NYEKUNDU** kikundi) haitatekeleza uingiliaji kati bila kujali jinsi programu hiyo ni rafiki na ina ufanisi kiasi gani. Walimu hawa wanaweza kuwa karibu na kumaliza ajira yao na wameona mbinu nyingi mpya zikija na kuondoka, au sababu zingine zinaweza kudhoofisha motisha zao ili kujaribu mbinu mpya, kama vile malipo yanayochukua muda mrefu au malipo ya chini. Kimsingi, mara nyingi programu za FLN hutumia muda mwingi na rasilimali kwa sehemu hizi mbili za idadi ya walimu, licha ya ukweli kwamba bila kujali mpango huo unafanya nini, kutakuwa na athari ndogo kwao, ama chanya au hasi.

Kwa upande mwingine, idadi kubwa ya "walimu wanaobadilika" huwakilisha idadi ya walimu ya kati (the **NJANO** block). Hawako kinyume na programu, na wataitekeleza iwapo mambo kadhaa yataboreshwa. Mifano ya mambo ya kuvutia yatakuwa:

- Programu ni rahisi.
- Inapunguza kiasi cha muda ambao mwalimu anatumia kuandaa andalio la somo.
- Walimu wanaweza kutambua athari katika kujifunza ndani ya wiki chache.
- Walimu wana ujuzi wa kutekeleza programu.
- Wasimamizi wanaimarisha hitaji la kutekeleza.

Kuzingatia walimu wanaobadilika, kama vile wapiga kura wanaobadilika, itahimiza wabunifu kukuza programu yao na kupunguza shughuli za ziada. Itashinda dhidi ya kuwa na seti ngumu ya vitabu vya kufundishia, miongozo ya mafunzo, vitabu vya tathmini endelevu, na maandalio ya somo (tazama Mwongozo wa 4, kwenye nyenzo). Programu ya Funda Wande nchini Afrika Kusini ilirahisisha programu yao, na kuwawezesha kuwalenga walimu wa kipengele cha njano, walimu wanaobadilika, kuliko kipengele cha kijani cha walimu walio tayari kutekeleza programu ngumu.

Analojia na utumiaji wa teknolojia katika elimu inaweza kuwa njia ya kufundisha. Waliotumia teknolojia mapema hawatapata shida katika teknolojia mpya kwa haraka na kuzitumia teknolojia hizo kwa kiwango cha juu. Ikilenga programu kubwa na ya kidigitali katika kiwango cha kuvutiwa kwao, hata hivyo, italeta tatuzi zilizo ngumu sana kuweza kutekelezwa na mwalimu wa kawaida katika mfumo, ambaye hajazoea vifaa vya kielekroniki vigumu. Kwahiyo, zingatia kurahisisha uingiliaji kati ili kuwalenga vema "walimu wanaobadilika" na kuza uwezekano kwamba waone programu kuwa ina ufanisi na inawezekana.

**KIELELEZO CHA 1: MODELI YA WALIMU "WANAOBADILIKA"**

**Utekelezaji wa kiwango kikubwa – Wapiga kura Wanaobdilika?**

| Waliovutiwa sana na kiko tayari kujaribu uingiliaji kati mpya hata kama ni ngumu | Watatekeleza programu iwapo masharti yatawavutia | Hawatatekeleza uingiliaji kati kwa sababu yoyote ile |
|---|---|---|
| ↑ | ↑ | ↑ |
| Onyesho kwa wafadhili | Msisitizo wetu wote unapaswa kuwa hapa | Je, tunapaswa kuwa na wasiwasi kuhusu haya? |

## HITIMISHO

**Kutambua kiasi ambacho viongozi wa serikali wanaweza kushawishi programu za FLN, na kuweka ushawishi huo katika matumizi mazuri, kunaweza kufanya programu kuwa na athari kubwa zaidi. Kwa upande mwingine, ni rahisi kusema kwamba serikali huongoza programu ya FLN na kwamba walimu wameichukua. Ngumu zaidi—lakini pia yenye faida zaidi—ni kupitia mchakato wa kuendeleza usimamizi wa serikali kwa njia ambazo zitaboresha athari na kudumu zaidi ya muda rasmi wa programu. Hii ni njia muhimu ili kuhakikisha uendelevu wa kweli, kwa sababu programu zinazoanza na usimamizi na uingiliaji kati wa serikali na kuwa michakato ya serikali zina uwezekano mkubwa si tu kuwa na ufanisi, lakini pia kudumu.**

Kuhusu alama katika mwongozo huu:

Huonyesha "Tahadhari Nyekundu": Kitu cha kukijua na kuchukua tahadhari, kwa sababu ni tatizo la kawaida

Huonyesah "Isiyojadiliwa": lazima kuwa nayo

## RASILIMALI

**Waziri Mkuu wa India Narendra Modi ametangaza ongezeko la kujikita katika msingi wa kusoma na kuhesabu**
https://www.youtube.com/watch?v=Y9JA7VK0e8o&feature=youtu.be&ab_channel=CentralSquareFoundation

**Rais wa Kenya Uhuru Kenyatta akiwa katika uzinduzi wa programu ya kitaifa ya kusoma ya Tusome (kwa Kiswahili)**
https://www.youtube.com/watch?v=3zh3xl2orB4&ab_channel=TeamUhuru

**Maoni ya Piper kuhusu mchango unaofaa wa wafadhili wa kimataifa na wataalamu wa kiufundi juu ya kutekeleza programu za elimu** https://doi.org/10.1007/s11159-016-9544-y

**Nyenzo ya uchoraji ramani ya kitaasisi ili kuelewa vema watendaji katika mfumo, kuanzia ukurasa wa 60.**
https://www.urc-chs.com/sites/default/files/urc-grn-lla.pdf

**Nyenzo rahisi ya uchoraji ramani ya kisiasa ili kuelewa muundo wa Wizara, katika ukurasa wa 21 na 22.**
https://pdf.usaid.gov/pdf_docs/PNACA721.pdf

**Mwongozo muhimu ili kuwaelewa walimu na mjadala wa kijamii unaohitajika ili kuzingatia mabadiliko ya walimu.**
https://dakar.iiep.unesco.org/sites/default/files/fields/publication_files/methodological_guide_for_the_analysis_of_teacher_issues_-_2010.pdf

**Miongozo Kamili ya Mfululizo wa Jinsi ya Kanuni za Ufundishaji:** https://scienceofteaching.site/how-to-guides/

MAREJELEO

1 Luis Crouch, *Systems Implications for Core Instructional Support Lessons from Sobral (Brazil), Puebla (Mexico), and Kenya* (RISE Insight Series, 2020/020, RISE Programme online, July 8, 2020). https://doi. org/10.35489/BSG-RISE-RI_2020/020
2 Central Square Foundation, "Indian Prime Minister Narendra Modi [India] on Foundational Literacy and Numeracy Mission and the Importance of Oral Reading Fluency," video (September 11, 2020): 2:01. https://www.youtube.com/watch?v=Y9JA7VK0e8o&feature=youtu.be&ab_channel=CentralSquareFoundation.
3 Pratham Education Foundation, *Annual Status of Education Report* (Rural) 2019: 'Early Years' (New Delhi, India: ASER Centre, 2020). http://img.asercentre.org/docs/ASER%202019/ASER2019%20report%20/aserreport2019earlyyearsfinal.pdf.
4 Uwezo, *Are Our Children Learning? Uwezo Kenya Sixth Learning Assessment Report* (Nairobi: Twaweza East Africa, 2016). http://www.uwezo.net/wp-content/uploads/2016/12/UwezoKenya2015ALAReport-FINAL-EN-web.pdf.
5 Piper, Benjamin. "International Education Is a Broken Field: Does Ubuntu Education Bring Solutions?" I*nternational Review of Education* 62, no. 1 (2016): 101–111. https://doi.org/10.1007/s11159-016-9544-y
6 Joseph DeStefano and Luis Crouch, Education Reform Support Today (Prepared for USAID under the Educational Quality Improvement Program 2 (EQUIP2), Cooperative Agreement No. GDG-A-00-03-00008-00. Washington, DC: Academy for Educational Development (AED), 2006). https://pdf.usaid.gov/pdf_docs/PNADQ913.pdf.
The original Education Reform Support series is available for download: Prepared for USAID under the Advancing Basic Education and Literacy (ABEL) program, Contract Numbers HNE-5832-C-00-4075-00 (core) and HNE-5832-Q-4076-00 (requirements). Washington, DC: Academy for Educational Development and Research Triangle Institute. Volume One: Overview and Bibliography. Luis Crouch and F. Henry Healey

Hati hii imepewa leseni chini ya Leseni ya Kimataifa ya Hatimiliki Inayoruhusu Umma Kunakili, Kusambaza, na Kuboresha Maudhui Jinsi Wapendavyo 4.0.

Mwongozo umeandikwa na **Dkt. Benjamin Piper**